Tangazo la Serikali Na ..... La Tarehe .....

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA, SURA YA 290

_____

SHERIA NDOGO

_____

(Zimetungwa chini ya kifungu cha 6(1)(u) na 16(1)

_____

SHERIA NDOGO ZA (USHURU WA HUDUMA) ZA HALMASHAURI YA JIJI LA DAR ES SALAAM ZA MWAKA 2020

Jina na Tarehe ya kutumika

1. Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za (Ushuru wa Huduma) za Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam za Mwaka 2020 na zitaanza kutumika baada ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.

Matumizi

2. Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo la mamlaka ya Jiji la Dar es Salaam.

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa pale itakavyoelekezwa vinginevyo maneno haya yatakuwa na maana zifuatazo:-

"*Afisa Mwidhiniwa*" Maana yake ni Afisa yeyote wa umma atakayekuwa anatekeleza majukumu ya Sheria Ndogo hizi.

"*Biashara*" Maana yake ni shughuli ya kibiashara au uchumi inayojihusisha na shughuli za kibenki, kifedha kwa kutumia njia za kielektroniki na zisizo za kielektroniki pamoja na nyingine zenye miamala ya kifedha.

"*Halmashauri*" Maana yake ni Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam.

"*Hesabu za Biashara*" Maana yake ni taarifa ya hesabu za biashara kwa kipindi kinachoishia kutoa taarifa hizo.

"*Mkurugenzi*" Maana yake ni Mkurugenzi wa Jiji au mtu yeyote aliyekasimiwa kutekeleza majukumu yake.

"*Mlipa Ushuru*" Maana yake ni mtu, kampuni au taasisi inayomiliki biashara.

"*Ushuru*" Maana yake ni ushuru wahuduma utakaotozwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

"*Wakala*" maana yake:-

(a) Ikitumika kwa maana ya taasisi au kampuni iliyoteuliwa na Halmashauri kwa ajili ya kukusanya ushuru wa huduma kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi itakuwa na maana hiyo;

(b) Ikitumika kwa maana ya tawi la biashara mama iko nje ya eneo la Jiji itakuwa na maana ya mfanya biashara.

"*Waziri*" maana yake ni Waziri Mwenye dhamana na Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Ushuru wa Huduma

4. (1) Halmashauri itatoza na kukusanya Ushuru wa Huduma kwa mtu, kampuni au taasisi inayofanya shughuli za kibenki kwa kiwango cha asilimia sifuri nukta mbili (0.2) ya mapato ukiondoa kodi ya ongezeko la thamani (VAT) na ushuru wa forodha (excise duty) yanayotokana na huduma au biashara zinazofanyika ndani ya eneo la Halmashauri.

(2) Bila ya kuathiri kifungu cha 4 (1) cha Sheria Ndogo hizi ukokotoaji wa ushuru wa huduma utafanyika kwa kuzingatia mchanganuo ulioanishwa kwenye **Jedwali la kwanza** la Sheria Ndogo hizi.

Wajibu wa kulipa Ushuru

5. Itakuwa ni wajibu wa kila mtu, kampuni au taasisi ya fedha kulipa Ushuru wa Huduma utokanao na utoaji wa huduma, kazi, mauzo ya bidhaa katika eneo la Halmashauri.

Taratibu za kulipa Ushuru wa Huduma

6. (1) Kila mtu, kampuni au taasisi inayotakiwa kulipa Ushuru wa huduma , atawasilisha kwa Halmashauri taarifa za hesabu za mauzo kwa kila miezi mitatu (3) na atalipa Ushuru wa Huduma kwa mujibu wa viwango vitakavyotokana na ukokotoaji wa hesabu hizo.

(2) Endapo Mlipa Ushuru yeyote atashindwa kuwasilisha taarifa sahihi za biashara kwa wakati, Mkurugenzi kwa maandishi anaweza kumtaka Mlipa ushuru huyo kuwasilisha taarifa hizo

ndani ya siku thelathini zinazohusu kipindi maalum cha hesabu zikionyesha kiasi na thamani ya huduma za kifedha zilizotolewa.

(3) Mkurugenzi au Afisa Mwidhiniwa anaweza kumtaka kwa maandishi mtu yeyote mwenye taarifa kuhusu mtu, kampuni au taasisi yoyote ya fedha inayopaswa kulipa ushuru kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi, kuwasilisha kwake taarifa ambazo zitatumiwa kama taarifa sahihi.

Uwezo wa kufanya ukaguzi

7. Mkurugenzi au Afisa Mwidhiniwa anaweza kuingia kwenye eneo lolote la Mlipa Ushuru kwa ajili ya kutafuta taarifa au kuchunguza hesabu, vitabu au taarifa zozote kama ataona inafaa na kufanya uchunguzi wa taarifa zinazohusu ushuru.

Makosa

8. Itakuwa ni kosa kwa Mtu, kampuni au taasisi yoyote ya biashara endapo-

(a) Itawasilisha taarifa za uongo kuhusu mapato;
(b) Itashindwa kulipa ushuru wa huduma kwa wakati;
(c) Itamzuia Mkurugenzi au Afisa Mwidhiniwa kutekeleza majukumu yake; na
(d) Itafanya jambo lolote kinyume cha Sheria Ndogo hizi.

Kufifilisha kosa

9. Mkurugenzi anaweza kufifilisha kosa endapo Mkosaji atakiri kosa kwa hiari yake mwenyewe na kukubali kulipa faini kiasi kisichopungua Shilingi Laki Mbili (200,000/=) na kisichozidi shilingi Laki Tano (500,000/=) baada ya kujaza fomu iliyoainishwa katika **Jedwali la Pili** la Sheria Ndogo hizi pamoja na kulipa kiasi cha ushuru anaodaiwa.

Adhabu

10. Mtu yeyote atayekwenda kinyume na masharti ya Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa na endapo atapatikana na hatia atatozwa faini isiyopungua shilingi Laki Mbili (200,000/=) na isiyozidi shilingi Milioni Moja (1,000,000/=) au kifungo kisichopungua miezi kumi na mbili na kisichozidi miezi ishirini na nne au vyote kwa pamoja faini na kifungo.

Kufutwa Tangazo la Serikali Na. 42 la tarehe 24/02/2017

11. Sheria Ndogo za (Ushuru wa Huduma) za Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam za Mwaka 2017 zinafutwa.

JEDWALI LA KWANZA
(Imeundwa chini ya kifungu cha 4 (2))

HALMASHAURI YA JIJI LA DAR ES SALAAM

FOMU YA UWASILISHAJI WA USHURU WA HUDUMA ITAWASILISHWA KILA ROBO YA MWAKA

SHERIA YA FEDHA YA SERIKALI ZA MITAA YA MWAKA, SURA YA 290 R.E 2002

JINA LA TAASISI: ……

UKOKOTOAJI WA MAPATO GHAFI KWA KIPINDI CHA MIEZI MITATU (ROBO) YA MWEZI WA …….....HADI……..…….

MAELEZO	Kiasi (TShs)
1. MAPATO YATOKANAYO NA FAIDA YANAYOPOKELEWA	
a. FAIDA – Mikopo ya awali & Overdraft	
b. FAIDA – Mikopo ya Banki kwa Banki	
c. FAIDA – Uwekezaji kwenye Amana za mikopo	
d. FAIDA – Yatokanayo na uwekezaji Serikalini	
e. FAIDA Salio toka Banki Kuu	
f. FAIDA – Salio kutoka Banki zangine	
g. FAIDA – Nyinginezo **(Zitaje)**	
JUMLA YA MAPATO YATOKANAYO NA FAIDA YANAYOPOKELEWA ……. A	
2. GHARAMA ZITOKANAZO NA FAIDA ZINAZOLIPWA	
a. FAIDA – Fedha za Wananchi walizowekeza Banki	
b. FAIDA – Fedha za Serikali walizowekeza Banki	
c. FAIDA – Fedha lilizowekwa na Banki Nyingine	
d FAIDA – Mikopo toka Banki Nyingine	
e. FAIDA – Gharama Nyinginezo **(**Zitaje**)**	
JUMLA YA GHARAMA ZA FAIDA INAYOLIPWA B	
3. MAPATO KAMILI BAADA YA KUTOA MALIPO C= A-B	
4. MAPATO MENGINEYO YASIYOTOKANA NA FAIDA	
a. Mapato yanayotokana na Biashara ya Fedha za Kigeni Faida **(Hasara)**	
b. Asilimia inayopokelewa kama wakala wa Biashara za nje ya Nchi	
c. Mapato ya tozo la Akaunti ya Biashara	

d. Mapato mengineyo yatokanayo na Uwakala na Huduma za malipo	
e. Biashara ya uwekezaji wa Amana Faida /**(Hasara)**	
f. Mapato tokana na udhamini & Akaunti za Amana	
g. Biashara itokanayo na dhahabu Faida **(**Hasara**)**	
h. Mapato mengineyo	
i. Mapato yatokanayo na Ukodishaji wa Maeneo na Mali	
j. Mapato ya gawio kwenye uwekezaji	
5.MAPATO MENGINEYO YASIYOTOKANA NA FAIDA D	
6.JUMLA YA MAPATO YOTE E=C+D	
KIWANGO CHA TOZO 0.2%	
USHURU WA HUDUMA UNAOLIPWA 0.2%*E	
7 .MAPOKEZI YA FEFHA	
a.Jumla ya mapokezi yote ya Dar es Salaam Matawi na Makao Makuu	
B.JUMLA KUU YA MAPOKEZI YA TAASISI	

ANGALIZO:-
FOMU HII IJAZWE KWA USAHIHI NA IWASILISHWE PAMOJA NA MALIPO YA HUDUMA ZA JIJI IKIWA NI PAMOJA NA TAARIFA ZA MAHESABU YA FEDHA YA KIPINDI HUSIKA
Imeandaliwa na; Jina ……..… Cheo …… Saini ……... Tarehe ……...

Imepitishwa na; Jina ……..… Cheo …… Saini ……... Tarehe ……... Imeidhinishwa na; Jina ……..… Cheo …… Saini ……... Tarehe ……...

JEDWALI LA PILI

HATI YA KUKIRI NA KUFIFILISHA KOSA

(Chini ya kifungu cha 9)

Mimi ……..……mkazi wa Mkoa wa …… nakiri mbele ya ……..……..ambaye ni Mkurugenzi wa Halmashuri ya Jiji la Dar es Salaam, kwamba mnamo tarehe …… ya Mwezi ……. Mwaka 20…..… nilitenda kosa la kukiuka masharti ya kifungu cha …… cha Sheria Ndogo za (Ushuru wa Huduma) za Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam za Mwaka 2019.

Kwa Mamlaka aliyopewa Mkurgenzi wa Jiji, Niko tayari kulipa kiasi cha …… ninachodaiwa kama faini na hasara niliyosababisha.

NATHIBITISHA KWAMBA MAELEZO HAPO JUU NI YA KWELI NA NIMEYATOA KWA HIARI YANGU KADRI YA UFAHAMU WANGU

Leo tarehe ……Mwezi ……..Mwaka, ……

Jina: ……. Saini: …….

Mbele ya: *(Afisa aliyemkamata mtenda kosa)*

Jina: ……. Saini: …….

TAMKO LA MKURUGENZI

Kwa mamlaka niliyopewa na Sheria Ndogo nafifilisha kosa lako na kukuamuru Ndugu …….. kulipa faini ya shilingi za kitanzania ……..……. (Tshs. ……..) ikiwa ni adhabu kwa mujibu wa kifungu cha …….. cha Sheria Ndogo hizi TS. Na. ……./20……

Jina: ……..

Saini: ……. (*muhuri)*

Cheo: …….